Sitageuka Nyuma Kamwe

Yajue Maarifa Yatakayokuweka Huru

Jegi Nimuka Bassu

Jegi Nimuka Bassu

Sitageuka Nyuma Kamwe

© 2021 Jegi Nimuka Bassu

Haki zote za kitabu hiki zimehifadhiwa. Huruhusiwi kunakili au kudurufu sehemu yoyote ya kitabu hiki bila idhini ya mwandishi. Kufanya hivyo itakuwa ni ukiukwaji wa haki za mwandishi na mchapaji. Ikigundulika hatua za kisheria zitachukuliwa.

Mawasiliano na Mwandishi:
Jegi Nimuka Bassu
S.L.P. 710, Tukuyu Mbeya.
Simu +255 754 553 303
Barua pepe: iliketanz@gmail.com

Kimesanifiwa na Kupangwa na **Maige Gambishi**
Kigoma, Tanzania
+255 752 336 214
mygmoses@gmail.com

Cover Design: Mwalimu Bassu

KUHUSU MWANDISHI

Jegi N. Bassu ni Mjasiriamali mwenye uzoefu wa miaka mingi sasa. Historia yake ya Ujasiriamali ilianza akiwa darasa la nne (mwaka 1993) akiwa anasimamia biashara ya duka la baba yake.

Hakuishia hapo bali aliweza hata kuuza Big G (Bazoka) wakati wa mapumziko shuleni akiwa shule ya msingi. Kwa maoni yake, anasema **aliona kuwa muda huo wa mapumziko usipotee bure**.

Akiwa kidato cha sita Songea Boys (2003) aliweza kufanya biashara ya ujumbe mfupi wa maneno kwenye simu alimaarufu kama sms. Kipindi hicho hakukuwa na sheria inayozuia simu shuleni. Kwa hiyo akaitumia vyema fursa hiyo ya uhitaji wa mawasiliano akiwa shuleni. Ilikuwa ni fursa kwa sababu ni Jegi na mwanafunzi mwingine mmoja tu ndio walimiliki simu kipindi hicho kati ya wanafunzi zaidi ya 800 wa shule hiyo.

Likizo zake nyingi alizitumia kwa ajili yakukuza biashara ya familia yao na aliweza kusimamia ujenzi wa vyumba zaidi ya 10 vya nyumba ya kulala wageni ambayo familia yao ilijenga. Alifanya hayo akiwa bado ni mwanafunzi wa sekondari.

Akiwa anasoma Stashahada (Diploma) ya Ualimu katika Chuo cha Ualimu Tukuyu (2005-2007), Jegi aliweza kufanya biashara ya vocha za simu kwa njia ya VodaFASTA. Alifanya biashara hiyo kwa jumla na rejareja. Kwa jumla aliweza kuwajumlishia wanachuo wengine ambao nao pia waliweza kuuza vocha kwa rejareja.

Kupitia biashara hiyo ya vocha chuoni, Jegi anasema kuwa ilimfanya mpaka akafahamika sana kwa wakufunzi na wanachuo kwa ujumla. Anasema kuwa mpaka Mkuu wa Chuo alikuwa ni mmoja ya wateja wake wakubwa wa vocha za kurusha.

Hamu yake ya kuyasaka mafanikio ilimfanya akajiunga na Chuo Kikuu cha SUA (Sokoine University of Agriculture) akisoma Shahada ya Ualimu na Kompyuta (*Informatics and mathematics*).

Chuoni hapo aliendeleza moyo wake wa ujasiriamali pale alipounda kundi la vijana watano waliojiita "*Computer doctors*" (2010-2013). Vijana hawa walishiriki vyema katika kufanya matengenezo madogo madogo ya kompyuta za wanachuo wenzao kwa gharama nafuu.

Mjasiriamali huyu amewahi kufundisha katika shule za sekondari za Iponjola (Mbeya), Ndembela (Mbeya) na Didas Masaburi (Chanika Dar-es-Salaam).

Ujasiriamali ndiyo umemfanya aanze kuandika vitabu mbalimbali vya Ujasiriamali, Elimu ya Fedha na Elimu ya Kujitambua. Mwandishi huyu pia hutoa semina

mbalimbali za elimu ya kujitambua, elimu ya fedha na elimu ya neno la Mungu sehemu mbalimbali nchini.

Mbali na uandishi wa vitabu, Jegi Bassu ni mwalimu wa elimu ya Kompyuta kwa KISWAHILI katika Mtandao wa **YouTube**. Chaneli yake inaitwa "**MWALIMU BASSU**".

Jegi Bassu (ambaye kwa jina la ubatizo ni **James**) amemuoa Grace na wamejaliwa kupata watoto watano; Samwel, Eva, Elisha, Nathanael na Brighton.

Mawasiliano na Mwandishi
+255 754 553 303

Shukrani

Shukrani za kwanza ziende kwa Mungu Muumba wangu kwani bila yeye kuamua kuniumba na kunijaalia maarifa kazi hii isingewepo.

Shukrani za pili ni kwa wazazi wangu; baba yangu **Bassu Nimuka Shindai** (Mungu amuweke mahali pema peponi) na mama yangu **Maria Magomasi**. Juhudi zao za kutaka nisome ili nije kulitumikia Taifa letu la Tanzania na dunia kwa ujumla hakika zimezaa matunda.

Shukrani za pekee ziende kwa walimu wangu wote katika hatua mbalimbali za elimu nilizopitia; katika elimu rasmi na elimu nje ya shule. Mungu awabariki sana walimu wangu.

Pia natoa shukrani kwa familia yangu, ndugu zangu, jamaa na marafiki. Bila wao na jitihada zao kuniimarisha naamini baadhi ya mambo niliyoyaandika humu nisingekuwa na ujasiri huo. Mungu aendelee kuwatia nguvu.

Bila kukusahau wewe unayesoma kitabu hiki, nakushukuru sana kwa kuwa naamini unanijali na kuzidi kuniombea.

Dibaji

SITAGEUKA NYUMA KAMWE ni kitabu kizuri kwa kila mtu mwenye kiu ya kupokea mabadiliko **chanya** katika maisha yake.

Kitabu hiki ni kitabu kinachoeleza uhalisia wa maisha ya kila siku. Kinaeleza uhalisia wa maisha ya watu walioko njiapanda katika maisha yao, kinatoa uhalisia wa maisha ya watu wanaohitaji mafanikio na kinatoa mwongozo wa kufikia ndoto kuu katika maisha.

Kitabu hiki kimekuja katika wakati mwafaka ambapo watu wengi wanafikiri kwamba suala la kufanikiwa hutokana na miujiza, wakati wengine wanapoamini kwamba suala la kufanikiwa ni matokeo ya Mtu kupitia njia zisizo halali.

Kitabu hiki kimekuja wakati ambapo watu wengi hawajatambua kusudi la kuumbwa kwao.

Kitabu hiki kimekuja wakati ambapo watu wengi wanahisi kwamba wameumbwa kuja kuwa wafuasi na watumwa wa watu fulani wakati lengo la Mungu kumuumba Mwanadamu lilikuwa ni kumfanya

Mwanadamu atawale kwenye karama ambayo alipewa kabla hajazaliwa (Mwanzo 1:26).

Kitabu hiki kimekuja wakati ambapo watu wengi wanashindwa kufanya mabadiliko chanya katika maisha yao. Mabadiliko kutoka kuajiriwa na kujiajiri, mabadiliko kutoka kuwa mfuasi wa watu na kuwa mfuasi wa kile Mungu alichokitoa kwa mtu.

Maarifa yaliyomo kwenye kitabu hiki yatamfanya msomaji atoke kwenye njiapanda ya maisha yake, yatamwezesha kutambua thamani yake, yatamwezesha kutengeneza fursa kuliko kutafuta fursa, yatamsaidia kutambua Kanuni za mafanikio kuliko kuamini katika miujiza.

Kitabu hiki kitamsaidia msomaji atoke kwenye hali ya kuwa mtumwa wa fedha badala yake fedha imtumikie.

Kitabu hiki kitamsaidia msomaji kuweza kupanga malengo yanayotimia.

Kitabu hiki kitamsaidia msomaji kuweza kutambua nguvu yake ya ndani na kusudi la kuumbwa kwake.

Kuanzia siku nilipomfahamu ndugu **Jegi Nimuka Bassu** nimegundua nguvu kubwa ndani yake.

Kwanza ni mtu anayependa kujifunza sana na anapenda kile alichonacho kiwe msaada kwa watu wanaomzunguka, ni mtu anayependa kuona watu wakifikia ndoto zao, ni mtu anayependa kuona watu wakiwa huru kwenye kazi zao, wakiwa huru kifedha na wakifanya yote katika njia inayompendeza Mungu. Mara nyingi haamini kwamba riziki yake inaweza kurudishwa nyuma na mwanadamu, anaamini kwamba mtu yeyote akitumia uwezo aliopewa na Mungu ndani yake hawezi kurudi nyuma kamwe.

Katika maisha yangu huwa naamini kwamba ***Elimu haina Mwisho*** ndiyo maana naendelea kujifunza kupitia vijana wenye fikra chanya katika kuliendeleza Taifa na Dunia kwa ujumla wake.

Naamini kwamba kila mtu mwenye kiu ya mabadiliko chanya atamtumia ndugu Jegi Nimuka Bassu kwa manufaa zaidi.

Aidha, nitazidi kumuombea kwa Mungu ili azidi kumtia nguvu, uwezo, maarifa na moyo wa kuendelea kuitumikia jamii yake, lakini pia Mungu awawezeshe watu wengi kunufaika na karama ya Jegi Nimuka Bassu.

Mwl. Jonathan Kwizera,
Mkurugenzi Ndoto Yangu Academy.
Dar es Salaam.
kwizerajonathan99@gmail.com
+255 627 177 566

UTANGULIZI

Binadamu ameumbwa na Mwenyezi Mungu ili awe **kiumbe huru**. Awe na uhuru wa kufanya maamuzi yake binafsi (pasipokuvunja sheria) na si kwa kupangiwa na mtu mwingine.

Mwandishi Vincent Mabula Jilala, Katika kitabu chake cha "Mwanzo wa Kuwa Tajiri" aliandika kuwa, "*Kuna njia mbili mtu anazoweza kuchagua kupita, kuna njia ya umaskini na kuna njia ya utajiri*." Akaongeza kuwa, "*usipochagua njia ya utajiri moja kwa moja utakuwa umechagua njia ya umaskini*."

Kuna hofu nyingi zinazowazuia watu wengi kuchagua kuwa matajiri. Baadhi yake ni ukosefu wa maarifa na kukwepa kulipa gharama inayohitajika ili apite kwenye njia hiyo. Hivyo, badala yake, hujikuta wanaangukia moja kwa moja kwenye umaskini.

Ni kwenye huo umaskini ndiyo mtu hujikuta akilazimika kuwa **mtumwa wa mtu mwingine** huku akipoteza uwezo wake wa kuamua na kuanza kuamliwa kwa kila jambo. Ndiyo! Ataamuliwa kila jambo kwa sababu yeye ni mtumwa tayari.

Mimi na wewe tu watoto huru wa Ibrahimu na mama yetu Sara. Ndiyo maana Biblia inaendelea kutukumbusha kuwa, "*Ndiposa, ndugu zangu, sisi si watoto wa mjakazi, bali tu watoto wa huyo aliye mwungwana*." (Wagalatia 4:31)

Katika toleo la Biblia la GNB (Good News Bible), tunasoma kuwa, "*So then, my brothers and sisters, we are not the children of a slave woman but of a free woman*." (Galatians 4:31)

Ni aibu mtoto wa mama huru kuingia utumwani. Na ikitokea ukaingia utumwani basi usizoee hali hiyo na wala usikae miaka yako yote katika utumwa huo. **Pambana usiku na mchana ili ujinasue.**

Nimeandika kitabu hiki baada ya kuacha ajira ya Ualimu Serikalini zaidi ya mwaka mmoja sasa. Maamuzi yangu niliyafanya si kwa ajili ya faida yangu pekee bali kwa ajili ya faida ya jamii nzima. Mimi kama Mwalimu nina wajibu wa kuifundisha jamii katika nyanja mbalimbali za maisha.

Nilipokuwa bado mwajiriwa nilikua nakosa sauti ya kumwambia mwanafunzi wangu aliyehitimu chuo kikuu,

na kubaki mtaani, kwamba ajiajiri wakati mimi mwalimu wake sijafanya hivyo.

Nilipoamua kuacha ajira Serikalini sikurejea tena, japo nilipewa fursa hiyo. Kwa nini sikugeuka nyuma? Biblia Takatifu inatuambia kuwa mke wa Lutu alipogeuka nyuma aligeuka kuwa jiwe la chumvi. Tunasoma kuwa, "*Lakini mkewe Lutu akatazama nyuma yake, akawa nguzo ya chumvi*" (Mwanzo 19:26). Hivyo, mimi sikugeuka na kamwe sitageuka nyuma. Sitaki kugeuka jiwe.

Lakini vile vile, Biblia Takatifu inatuambia kuwa ukiamua kufanya jambo fulani, si busara kurudi au kurejea nyuma: "*Yesu akamwambia, Mtu aliyetia mkono wake kulima, kisha akaangalia nyuma, hafai kwa ufalme wa Mungu*." (Luka 9:62)

Nilikuwa nimechagua kujiajiri na baadaye kutengeneza ajira ili niweze kuajiri watu wengine wanisaidie kutimiza ndoto zangu. Ndoto za kuwa huru kiuchumi, kimwili na kiroho.

Maana uhuru ndio kila kitu. Wahenga walisema, "*Uhuru jambo halisi kuukosa ni utumwa*." Sasa kama nimetambua kuwa mimi ni mwana wa mama huru kwa nini niwe mtumwa, nikakosa uhuru wangu?

Hivyo, nisingegeuka nyuma, yaani nilijiepusha kabisa kuwa na nia mbili; nia ya kujiajiri na nia ya kuajiriwa. Nilijiepusha kuwa na nia mbili maana mbali ya Biblia kukataza, hata Wahenga wameasa pia. Wahenga walisema "*Nia mbili hazienziani*", na wakaongeza kuwa "*Mtaka yote kwa pupa hukosa yote*". Sikutaka kukosa yote, nikaamua kukomaa na moja, la kujiajiri.

Nikaamua kusonga mbele huku nikipambana kwa kuweka malengo, kuandaa mikakati ya kutekeleza hayo malengo na kujifunza nidhamu binafsi ya hali ya juu ili kuweza kujisimamia mwenyewe kufanyia kazi mikakati yote niliyojiwekea ili niitimize kwa wakati wake.

Kama mimi nimeweza nawe pia unaweza kuchukua maamuzi thabiti katika kutimiza ndoto zako na ukakataa kugeuka nyuma.

Katika sura zifuatazo nitataja na kufafanua kwa undani baadhi ya sababu zilizonifanya nisigeuke nyuma, bali nikaendelea kusonga mbele. Sasa endelea…

Always Aim at High.